**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUYENZI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU- – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu w Shule: 0784 480 914**

**Makamu wa mkuu wa shule:0782 577 577**

**Mhasibu 0625 815 407**

**Shule ya Sekondari MUYENZI**

**S.L.P. 05,**

**RULENGE - NGARA**

**...........................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ...............................**
**S.L.P .........................**
**.......................................**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUYENZI HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA MKOA WA KAGERA MWAKA ................**

**1.** Nanafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka .......... na atasoma tahasusi ya .................…

Shule ya Sekondari MUYENZI ipo umbali wa Kilometa 52 Kusini Magharibi mwa Mji wa NGARA. Usafiri wa basi kutoka mjini NGARA unapatikana katika kituo cha mabasi NGARA Nauli ni Shilingi 8000. Kama unatokea Mwanza panda mabasi ya Zube au Nyehunge na shukia Mji mdogo wa RULENGE. Nauli ya pikipiki toka RULENGE mpaka shuleni ni shilingi 5000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe .............. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ................... Masomo yataanza baada ya wiki moja tangu tarehe ya kuripoti.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 SARE ZA SHULE**

i. Sare ya shule hii ni sketi za rangi ya DARK BLUE mbili ( **KITAMBAA KIZITO ORIGINAL AINA YA <u>KRETA</u>)** Mshono wa marinda na marinda hayo yawe 12 au 16. Sketi iwe ndefu inayogusa kifundo cha mguu ( Tazama kimbatisho 1.1. **SKETI FUPI HAZITAPOKELEWA.** Wanafunzi wa Kiislamu nao watavaa sketi ndefu na sio suruali. Piga simu kwa mkuu wa shule kupata maelekezo endapo utapata changamoto yoyote au kutaka kupata ufafanuzi zaidi. Aidha belt za sketi ziwe na upana wa Inch 1.5 na lisilozidi Inch 2.

ii. **<u>Mashati mawili ya kushona</u>** ya rangi nyeupe yenye mikono mirefu(**<u>AINA YA KITAMBAA NI HALUA</u>**) na mashati hayo yawekewe alama ya namba Tano ya kirumi mabegani. Alama hiyo inawekwa kwa kitambaa Cha rangi ya dark blue.Ukipata changamoto ya kujua aina za vitambaa vya sare za shule piga simu kwa Mkuu wa shule kwa msaada zaidi. Nguo zote ziwekewe alama ya uambulisho, ikitokea imepotea iwe rahisi kuitafuta.

iii. Rangi ya Hijabu ya kuvaa darasani (Juba) kwa wanafunzi wa kiislamu ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. Ziwe mbili.

iv. Sare za Michezo ni
(a)Jezi ya rangi ya blue( tishet na kaptula yake)
(b) Track suit za rangi ya dark blue yenye nembo ya shule. ( Koti na suruali yake)

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na shingo fupi. Visiwe vya kubadili rangi (dye)

vi. Soksi nyeupe jozi tatu (stockings)

vii. Sweta mbili rangi ya LIGHT BLUE yenye nembo ya shule.

viii. T-shiert za shule rangi ya LIGHT BLUE yenye nembo ya shule.

ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni:

(a) Magauni mawili ya rangi ya **<u>pink</u>**,mshono wa marinda. Liwe na mikono mirefu, Magauni yawe marefu yanayogusa kifundo cha miguu. KITAMBAA cha magauni hayo kiwe **<u>kizito</u>**.

(b) Sketi Moja ya rangi ya kijani kibichi itakayovaliwa na tisheti yenye nembo ya shule. Tazama picha iliyoambatanishwa kwenye fomu hii. Kuwa makini na vitambaa vilivyoelekezwa na urefu unaotakiwa ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza.

(c) Pia hijabu za kushindia jioni ziwe mbili za rangi ya light blue ( Tazama kiambatisho 1.2)

x. Tai Moja ya dark blue ya pundamilia yenye nembo ya shule.

**2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-**

i. Madaftari makubwa ( counter books) kumi.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka. Aina ya ream ni DOUBLE A
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro la futi mbili na nusu aina ya Victoria au super banco. Kwa wanaotoka mbali maduka ya jirani na shule wanauza kwa TSH 55,000/.
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe,kitenge au Taulo la kuogea
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe na chupa ya kubebea maji ya kunywa).
x. Ndoo 2 kubwa zenye mifuniko na beseni
xi. Kotama 1,sabuni ya maji Lita 5, ufagio mmoja(1) wa ndani na mmoja(1) wa nje( chelewa wa mti)na squizer 1
**xii. Bima ya Afya (50,400) NI LAZIMA SIO HIARI. ITAKAGULIWA ATAKAPORIPOTI SHULENI.**
**xiii. Begi moja la kubebea madaftari.**

**2.3 MICHANGO MBALIMBALI**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Tafadhali lipa kupitia akaunti ya shule ifuatayo kwani pesa taslimu (cash) hazitapokelewa. Kumbuka kuandika majina kamili ya mwanafunzi na aje na risiti ya benki.

**JINA LA AKAUNTI NI: SHULE YA SEKONDARI MUYENZI**

**AKAUNTI NAMBA: 32101200060**

**BENKI: NMB**

**TANBIHI: Usiweke benki pesa nyingine yoyote tofauti na hiyo iliyoainishwa kwenye jedwali hapo juu. Pesa za matumizi binafsi ya mwanafunzi, nauli na mambo mengine zitumwe kwa mhasibu wa shule. Hakikisha umechukua namba ya mhasibu uliyoandikiwa hapo juu ili kuepusha usumbufu.**

## 3.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparations).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Endapo atahitaji kuwasiliana na wazazi atatatumia simu za shule zilizoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi kuwasiliana na wazazi au walezi wake.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NB:

i. **Wanafunzi waendapo likizo wanatakiwa kurudi shuleni kwa wakati na endapo atachelewa kurudi kwasababu zozote zile atatakiwa kuripoti shuleni na mzazi. Asipofanya hivyo atarudishwa nyumbani.**
ii. **Muda wa kuripoti shuleni baada ya kutoka likizo ni kuanzia saa1:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni, endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti ndani ya muda huo atahesabika kuwa mchelewaji kama wachelewaji wengine waliochelewa kuripoti shuleni. Hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.**
iii. **Kutakuwa na mahafali ya kidato cha Nne ............. na kidato cha Sita ................, wanafunzi wote watatakiwa kuchangia na kushiriki kwa pamoja katika mahafali hayo.**

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;
iv. Bima ya Afya.

MUYENZI TUNAAMINI KUWA UTAPATA ELIMU BORA NA KUWA MTU SAHIHI KWA JAMII YA KITANZANIA.

MUYENZI BILA DARAJA LA TATU,NNE NA SIFURI INAWEZEKANA,KARIBU UTIMIZE WAJIBU WAKO NA KUKAMILISHA NDOTO YAKO

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**




**KURUTHUM MINGA SAMSON**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0611054430/0784480914**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0624159005**
- **Mwandamizi Taaluma 0626818531**

## SHULE YA SEKONDARI MUYENZI

## FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE

***(Ijazwe kwa herufi kubwa na kurejeshwa kwa mkuu wa shule)***

i. Jina kamili (mwanafunzi)......................................................
Tarehe ya kuzaliwa …………... Wilaya ………….. Mkoa ................
Taifa …………. Dini RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecosten.k
Shule ya SEKONDARI unayotoka …………………….

ii. Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi ………………………….
Anwani yake…………………………….
Kazi ya baba/Mama/Mlezi…………………………...
Anwani yake………………………...
Namba ya simu…………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI.**

i. Mimi……………………………………………….nimeyasoma na
Kuyaelewa maelezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule ni nimekubali kuingia kidato cha TANO katika shule ya Sekondari Muyenzi kuanzia Tareh………………hadi nitakapomaliza kidato cha SITA .

ii. Kwa hiyo naahidi kwamba:-

(a) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.

(b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa shule na serikali ja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kama kushiriki migomo ,Fujo,makosa ya jinai n.k.

(c) Nitatunza mali za UMMA ambazo ni pamoja na majengo na samani,vitabu n.k
Tarehe ………….. Sahihi ya mwanafunzi.

(d). Naahidi kuripoti shuleni kwa wakati mara baada ya kutoka likizo kulingana na kalenda iliyowekwa na endapo nitachelewa nitawajibishwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za shule.

**AHADI YA MZAZI/MLENZI**

Mimi…………………… ambaye ni mzazi/mlenzi wa mwanafunzi………………… nina ahidi kwamba :-

i. Nitashirikiana na uongozi wa shule , walimu na watumishi wasowalimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya sekondari Muyenzi iwapo atashindwa kutii sheria hizo nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongonzi wa shule.
ii. Nitafanya kila niwezalo kuwezesha mwanangu kusoma kwa bidii kama ilivyoelekezwe na shule.

Sahihi …………. Tarehe……………
Namba ya simu ……………

NGARA DISTRICT COUNCIL

MUYENZI SECONDARY SCHOOL

**MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by Medical officer in respect of Muyenzi Secondary School student.(entarant)

2) Students full name……………………………………..
3) Sex……………………………..
4) HGB Test…………………………………..
5) STOOL Test: ……………………….
6) UPT ………………………..
7) T.B Test: ………………………….
8) EYE Examination: ……………………………..
9) E.N.T …………………………………..
10) CHEST ……………………………………………
11) ABDOMEN …………..

ADDITIONAL INFORMATION …………..

Physical defects or impairments, infection, chronic or hereditary (family disease).

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………...

I certify that I have examined the above student and discover that HE/SHE is Physically /NOT physically fit for further studies .

**OFFICIAL STAMP**

KIAMBATANISHO CHA MFANO WA SARE ZA SHULE



KIAMBATISHO 1.2 CHA MFANO WA HIJABU ZIVALIWAZO WAKATI WA MASOMO



KIAMBATISHO 1.3 MFANO WA SHAMBA DRESS ( SKETI ZA KIJAN)



KIAMBATISHO1.4 KIAMBATISHO KINACHOONESHA MFANO WA HIJABU ZIVALIWAZO BAADA YA MASOMO

